



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA TANO

24 JUNI 2010



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 24 JUNI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

106. MHESHIMIWA DK. FESTUS BULUGU LIMBU (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa walimu wa shule za msingi na sekondari hapa nchini:-

Je, kwa nini Serikali isisimamishhe kwa muda ujenzi wa shule mpya za msingi na sekondari.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:

107. MHESHIMIWA SALIM HEMED KHAMIS (CHAMBANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:- Vilabu vingi vya Mpira wa Miguu Duniani kama vile F.C. Barcelona vimepata mafanikio makubwa kwa kutumia vijana wake kutoka “Academy” badala ya kuendelea kununua wachezaji toka nje:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia uzoefu huo kuvishawishi vilabu vyetu vya mpira hapa nchini kuanzisha “Academy”.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

108. MHESHIMIWA PROF. RAPHAEL BENEDICT MWALYOSI (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kipindi cha mwezi Desemba, 2009 hadi Januari 2010 kiliambatana na matetemeko makubwa sana ya nchi (Magnitude) na kujirudia katika muda mfupi (high frequency) kwenye maeneo ya bonde la ufa hususan bonde la Ziwa Nyasa na hivyo kuleta hofu kwa wananchi wa maeneo hayo:-

Je, ni sababu zipi za Kisayansi zinazosababisha matukio hayo.

109. MHESHIMIWA LAUS OMAR MHINA (KOROGWE VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kwa muda mrefu kumekuwa na ahadi ya kusambaza umeme katika maeneo ya vijiji vya Dindia, Mkalamo katika Kituo cha Afya cha Rozimin, Kibaoni/Lusanga, Makumba, Kijango, Kwemazandu na Kijingu Moto:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa hasa ikizingatiwa kuwa njia kuu za umeme zimepita katikati/karibu na vijiji hivyo.

110. MHESHIMIWA TATU MUSA NTIMIZI (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 iliweka mkazo juu ya kupeleka umeme vijijini:-

Je, Serikali inasema nini juu ya mradi huu wa umeme katika vijiji vya Igalula ambapo hakuna kilichofanyika mpaka sasa, licha ya wataalam kuzunguka vijiji vya Jimbo hilo na kutambua sehemu za kupitishia umeme tangu mwaka 2006/2007.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

ORODHA YA NYONGEZA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA TANO

**OFISI YA BUNGE
S.L.P. 941
DODOMA**

24 JUNI 2010



ORODHA YA NYONGEZA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 24 JUNI, 2010

I. KAULI ZA MAWAZIRI:

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO.

**DODOMA
24 JUNI, 2010**

**DKT. T.D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**